DirectAid
ARAFAH ISLAMIC ENGLISH MEDIUM PRE AND PRIMARY SCHOOL
P.O.BOX 1028 - SINGIDA.
Mobile: TEL: 0742500268/0719162701. E-mail: arafahiemps@gmail.com

# FOMU YA MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE MWAKA 2025:

**KWA MZAZI WA ________________________________________ DARASA LA _____________**

## A. UTANGULIZI:

Kwa niaba ya Uongozi wa Shule ya **ARAFAH ISLAMIC ENGLISH MEDIUM PRE AND PRIMARY SCHOOL**. Tunapenda kutoa pongezi za dhati kwa mwanao kwa kuchaguliwa kujiunga na Shule hii Darasa la___________mwaka 2025. Hivyo tunakukaribisha kwa moyo mkunjufu kujiunga na kuwa miongoni mwa wanajamii wa **DIRECT AID SOCIETY.**

## B. AINA YA SHULE :

**ARAFAH ISLAMIC ENGLISH MEDIUM PRE AND PRIMARY SCHOOL**. Ni shule inayomilikiwa na Taasisi ya kiislamu ya **DIRECT AID SOCIETY.** Shule hii inaendeshwa kwa kufuata taratibu za Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, na maadili ya Kiislamu. Shule ni ya kutwa na bweni. Pia, ina mchanganyiko wa Wavulana na Wasichana. Nafasi za bweni ni kwa wanafunzi yatima tu. Si hivyo tu, tunatoa elimu kwa wanafunzi wa dini zote.

## C. MAHALI SHULE ILIPO:

Shule inapatikana Kijiji cha **Manga** kata ya **Mtipa** katika Halmashauri ya **Manispaa ya Singida** mkoa wa **Singida**. Umbali wa **Kilomita 11** kutoka **Singida mjini**, barabara kuu ya kuelekea Mwanza.

## D. TAREHE YA KUFUNGUA SHULE:

Shule itafunguliwa tarehe ___________________siku ya Jumatatu saa 1.20 asubuhi. Wanafunzi wote wanatakiwa kuripoti tarehe hiyo kwa ajili ya kusajiliwa.

## E. MASOMO YANAYOFUNDISHWA SHULENI:

Ni masomo yote ambayo yameainishwa katika Mtaala wa Tanzania kwa Shule za English Medium. Masomo ya ziada ni pamoja na Lugha ya Kiarabu na masomo ya Dini ya Kiislamu.

## F. MAZINGIRA YA SHULE:

Shule ina mazingira tulivu kwa mwanafunzi kujifunza, na Walimu mahiri tayari kwa kumuwezesha mtoto kupata elimu na maarifa muhimu kwa maisha yake.

## G. LUGHA INAYOTUMIKA KATIKA KUFUNDISHA:

Lugha inayotumika katika kufundishia ni lugha ya **KIINGEREZA** isipokuwa somo la Kiswahili, Lugha ya Kiarabu na Elimu ya Dini ya Kiislamu.

## H. MUDA WA KUINGIA NA KUTOKA SHULE:

- ✓ Wanafunzi wote wawe wamefika shuleni saa 1:20 asubuhi.
- ✓ Na wataruhusiwa kutoka shule saa 9:30 alasiri.

## I. KIWANGO CHA UFAULU.

Kiwango cha ufaulu kwa mwanafunzi kuingia darasa lingine ni wastani wa asilimia 75%. Endapo mwanafunzi atashindwa kufikisha wastani huo uongozi wa shule kwa kushirikiana na mzazi watashauriana kuandaa program maalumu ya kumwezesha mtoto kufikia ufaulu unaohitajika.

## J. KANUNI, MAADILI NA SHERIA ZA SHULE:

**(i) KANUNI ZA SHULE:**

Kila mwanafunzi analazimika kufuata Kanuni na Taratibu zilizowekwa na Wizara ya Elmu, Sayansi na Teknolojia zinazolinda uendeshaji wa shule nchini.

**(ii) MAADILI NA SHERIA ZA SHULE:**

Kila mzazi atambue kuwa shule hii inaendeshwa kwa maadili ya **KIISLAMU.** Hivyo wanafunzi ni lazima kuzingatia maadili ya kiislamu katika kila hatua ya maisha yao hapa shuleni, kama swala, stara, n.k. Kila mwanafunzi hatotakiwa kujihusisha na yafuatayo ambayo yanaweza kumpelekea mwanafunzi kuchukuliwa hatua za kinidhamu. Ambayo ni:

1. Wizi
2. Kutumia Lugha chafu na za matusi
3. Kuharibu mali ya Umma na Shule kwa makusudi.
4. Kuchezea au kuharibu Bendera ya Taifa au Picha za viongozi.
5. Utoro wa jumla au rejareja.
6. Ugomvi wa aina yeyote hususani kupigana.
7. Kutotunza usafi wa mwili na mavazi au kubadilisha mwili.
8. Kuleta vitu ambavyo havihusiani na masomo kama vile simu, redio, pesa, mapambo n.k.
9. Kutovaa sare kamili ya shule; ni marufuku kuvaa aina nyingine ya vazi isipokuwa sare ya shule.
10. Wanafunzi wote hawaruhusiwi kujipamba kwa poda, kupaka rangi kucha, hina, piko, kuvaa vibanio vya nywele, kuvaa hereni, bangili na kupaka wanja.
11. Mtoto yeyote ambaye hatovaa Kiislamu na kutokuwa na nidhamu ya kuvaa vizuri sare ya shule atarudishwa nyumbani.
12. Wasichana wanaruhusiwa kusuka nywele tano mpaka saba tu (mnyoosho) si ruhusa kumsuka mtoto mitindo yoyote ya nywele. Mwanafunzi atakaebainika kusukwa mitindo tofauti na maelekezo atachukuliwa hatua za kinidhamu.
13. Si ruhusa kujihusisha au kushiriki mapenzi kwa namna yoyote ile.
14. Si ruhusa kutembelea maeneo yasiyoruhusiwa, Kama majumba ya sinema, kumbi za starehe na vilabu vya pombe na vinavyofanana na hivyo.
15. Kutokufanya kazi za darasani au kazi nyingine yeyote atakayopewa na mwalimu.
16. Kukataa au kumgomea mwalimu kufanya adhabu.

## K. UHARIBIFU:

Mwanafunzi yeyote atakaebainika kufanya uharibifu wa mali za shule kama kuvunja kifaa cha shule, kupoteza, kuchora au kuandika katika kuta au uharibifu mwingine wowote ule mzazi atalipa gharama za uharibifu huo, na shule haitavumilia uharibifu wa aina yeyote ile utakaofanywa na mtoto kwa makusudi.

## L. VIKAO VYA WAZAZI:

Kutakuwapo na vikao vya wazazi ambavyo kila mzazi atatakiwa kuhudhuria kama vitavyoitishwa.

## M. AWAMU ZA KILIPA ADA NA HUDUMA ZINGINE NA TAARIFA ZA KULIPA

| NA | DARASA | ADA | CHAKULA | USAFIRI | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | KG 1 na KG 2 | 400,000 | 300,000 | 550,000 | 1,250,000 |
| 2. | 1, 2, 3, 5 na 6 | 500,000 | 300,000 | 550,000 | 1,350,000 |
| 3. | 4 na 7 | 530,000 | 330,000 | 826,000 | 1,686,000 |

## N. AWAMU ZA KULIPA ADA NA HUDUMA ZINGINE NA TAREHE ZA KULIPA

| N | CLASS | INSTALLMENTS | | | | | | | | | | | | | | TOTAL |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | JANUARY | | | BUS ON SATURDAY | TOTAL | MAY | | | BUS ON SATURDAY | TOTAL | JULY | | | TOTAL | |
| | | FEES | FOOD | BUS | | | FEES | FOOD | BUS | | | FEES | FOOD | BUS | | |
| 1 | K G 1 &K G2 | 150000 | 150000 | 200000 | | 500000 | 150000 | 100000 | 200000 | | 450000 | 100000 | 50000 | 150000 | 300000 | 1250000 |
| 2 | 1-2-3-5-6 | 200000 | 150000 | 200000 | | 550000 | 150000 | 100000 | 200000 | | 450000 | 150000 | 50000 | 150000 | 350000 | 1350000 |
| 3 | 4&7 | 250000 | 150000 | 200000 | 138000 | 738000 | 160000 | 100000 | 200000 | 138000 | 598000 | 120000 | 80000 | 150000 | 350000 | 1686000 |

**NB.**

Fedha yote ilipwe benki ya **CRDB, Account number** 0150077278900.

Jina la Akaunti ni **AFRICA MUSLIM AGENCY SINGIDA.**

Kisha mzazi awasilishe Slip ya malipo ya bank na atapatiwa risiti ya mkono shuleni.

- **Mzazi ambae hatakamilisha malipo yaliyoainishwa kwenye jedwali, mwanae hatapokelewa.**
- **Pia Rim 1 za A4 kwa mwaka kwa darasa la awali, I, II, III, V na VI.**
- **Darasa la Saba na darasa la nne wataleta rimu 2 kwa mwaka.**

## O. SARE YA SHULE

Shule haina utaratibu wowote wa kushona sare za shule. Hivyo mzazi utamshonea mwanao sare kwa utaratibu ufuatao:-

**WAVULANA:**

(i) Suruali rangi ya kijivu **jozi mbili.**
(ii) Sweta la kijivu.
(iii) Truck suit ya kijivu.
(iv) T. shirt ya Kijivu
(v) Nusu kanzu nyeupe ya mikomo mirefu yenye kola ya mviringo iliyozungushiwa draft nyeupe na blue shingoni na mikononi, **jozi mbili**.
(vi) Soksi nyeupe na viatu vyeusi visivyo na visigino virefu. Viatu viwe vya kufunga na kamba.
(vii) Raba nyeupe kwa ajili ya michezo.

**WASICHANA:**

(i) Suruali rangi ya kijivu **jozi mbili**
(ii) Gauni ya nusu kanzu inayofunika magoti rangi ya kijivu na mikono mirefu yenye drafti ya blue na nyeupe viganjani **Jozi mbili.**
(iii) Ushungi rangi nyeupe yenye draft nyeupe na blue juu.
(iv) Sweta la kijivu.
(v) Truck suit ya kijivu.
(vi) T. shirt ya kijivu.

(vii) Kitambaa cheupe cha kichwani.
(viii) Soksi nyeupe na viatu vyeusi visivyo na visigino virefu. Viatu viwe vya kufunga na kamba.
(ix) Raba nyeupe kwa ajili ya michezo.

## P. VIFAA VYA MASOMO:

Mzazi anawajibika kumnunulia mwanae vifaa vifuatavyo.

**CHEKECHEA: 1 (KG1)**

(i) Daftari za kurasa 200
- Mistari mikubwa na midogo 3
- Daftari isiyokuwa na mistari 2
- Daftari ya box 4

(ii) Penseli (H.B)
(iii) Kichongeo na ufuto
(iv) Rangi za kuchorea 1pc
(v) Begi la kubebea daftari

**CHEKECHEA: 2 (KG2)**

(i) Daftari za kurasa 200
- Mistari mikubwa na midogo 5
- Daftari isiyokuwa na mistari 1
- Daftari ya box 2

(ii) Penseli (H.B)
(iii) Kichongeo na ufuto
(iv) Rangi za kuchorea 1PC
(v) Begi la kubebea daftari

**DARASA LA KWANZA NA DARASA LA PILI**

(i) Daftari za kurasa 200 kama ifuatavyo:
- Mistari mikubwa na midogo 9
- Mistari ya kawaida 2
- Mistari ya box 1

(ii) Penseli
(iii) Rula
(iv) Kichongeo na ufuto
(v) Rangi za kuchorea
(vi) Begi la kubebea madaftari

**DARASA LA TATU MPAKA DARASA LA SABA.**

(i) Counter book 10 za quire 3
(ii) Kalamu yenye wino wa blue au Mweusi
(iii) Mathematical set
(iv) Rula
(v) Begi la kubebea madaftari ya shule

**VITABU VYA KIADA NA ZIADA VITAHITAJIKA KULINGANA NA MAELEKEZO YA MKUU WA SHULE**

## Q. USHIRIKIANO:

Wazazi/walezi wanatakiwa kutoa ushirikiano kwa uongozi wa shule wakati wote ili kumsaidia mtoto kufanya vizuri katika masomo yake.

Nakutakia utekelezaji mwema.

DAHARI HARIDI
MWALIMU MKUU